

Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA
KAZI YA KIMISHENI ULMWENGUNI KOTE

UBATIZO WA MUUMINI

Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu.
– Matendo 2:38

Katika karne ya 15 miali ya ufufuo ilipata joto na kusambaa kote katika bara Uropa wakati ambapo Mungu alianza kuwarudishia wanadamu ufaamu kamili wa kweli za Kibiblia. Hapo mbeleni ulimwengu ulikuwa katika hali ya giza (la usiku wa kiroho) kutokana na utawala wa giza wa Papa Mtakatifu, mkuu wa Kanisa la Roma, ambaye alikuwa ametia giza katika kweli zilizohubiriwa na kanisa la kwanza. Mabadiliko ya Kiprotestanti yaloanzishwa na Martin Luther huko Ujerumani mwaka 1517 yaliendelea kuenea wakati ambapo watu walianza kutambua upotovu wa dini ya Kikatoliki. Wengi wa Wakristo amba walileta mabadiliko hawakuwa na mwangaza kamili, lakini walikuwa wameanza kupata miali ya ukweli wa hapa na pale kuhusiana na maswala ya mafundisho ya kidini na tamaduni za Kikristo.

Conrad Grebel na Felix Manz walikuwa vijana wadogo amba walijifunza kutoka kwa mbadilishi wa mambo ajulikanaye kama Ulrich Zwingli wa huko Zurich, Uswisi. Lakini wao walihitlafiana na mbadilishi huyo kutokana na mazoea (ya miaka mingi) ya kanisa la Katoliki ya kubatiza watoto, jambo ambalo walionelea lilikuwa kinyume na

matendo ya Kanisa la Agano Jipy. Grebel na Manz na hata watu wengine walipata ufunuo kwamba ubatizo wa maji ulikuwa ufanyiwe tu kwa wale wambao walikuwa wametubu dhambi zao na kuzaliwa upya. Wao basi wakahubiri "ubatizo wa muumini" na wakafundisha kwamba wale amba walitaka kubatizwa walihitaji kukiri kibinasi kuhusu imani yao. Ndiposa



wakapinga swala la ubatizo wa watoto wachanga, kwa sababu watoto hao hawawezi kutubu wala kuamini, na basi hawastahili kubatizwa.

Kwa kweli hakuna Maandiko ambayo yanaunga mkono kubatizwa kwa watoto wachanga na hakuna mfano wa watoto wadogo wakibatizwa katika Biblia. Inaonekana kama kwamba ubatizaji wa watoto wachanga ulianza mwishoni mwa karne ya pili na ilipofikia katikati mwa karne ya tatu jambo hilo lilikuwa

limekubalika kanisani. Jambo hili likavuma sana kwa sababu kulikuwa na mafundisho ya uwongo yaliyosema kwamba watoto wangeishia jehanamu ikiwa hawangebatizwa, na kwamba ubatizo ultiwaokoa kutoka dhambini. Lakini ubatizo wa maji haumwokoi mtu kutoka dhambini. Watoto wachanga hawana hatia yoyote mbele zake Mungu kwa sababu wao hawajafanya dhambi yoyote kwa kusudia na wao watafika mbinguni ikiwa watakuwa huku wakiwa wangali wachanga.

Ubatizo wa watoto wachanga umeleta hasara kubwa kwa watu wengi. Ni jambo linalowafanya watoto kukua huku wakifiria kwamba wataenda mbinguni kwa sababu walibatizwa huku wakiwa watoto wachanga – hata ingawa sasa ni watu wazima na wanaishi maisha ya dhambi. Lakini watu wanastahili kuoshwa kwa damu ya Yesu, na kamwe hawastahili kushikilia mikongojo ya ubatizo wao wakiwa watoto wachanga eti utawaokoa.

Wale amba walismama wima dhidi ya ubatizo wa watoto na wakahubiri ubatizo wa waumini walijulikana kama Anabaptisti (maanake wanaobatiza mara ya pili). Ubatizo wa kwanza ulikuwa ule walipewa wakiwa watoto wachanga amba haukulingana na maandiko. Ubatizo wa pili "kubatizwa tena" ulikuwa ule ubatizo huku wakiwa waumini wa kweli wa Kristo.

(Inaendelea kutoka ukurasa 2)

MAMBO AMBAYO

BIBLIA

Inafundisha Kuhusu...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,

Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,

Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,

Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,

I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt.

25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Endelea kutoka ukurasa I)

Anabaptisti waliteswa na kanisa la Kikatoliki (kanisa la Roma) na pia wakateswa na Wakristo wa Kiprotestanti kutoptaka na wao kubatiza watu wazima. Hapo tarehe 7, Mechi, mwaka wa 1526 kamati iliyokutana Zurich ilipitisha sheria ambayo ilimhukumu yeoyote aliyebatiza au kubatizwa mara ya pili, auawe kwa kuzamishwa majini. Ndiposa Manz akawekwa korokoroni. Lakini punde tu alipoachiliwa yeye aliendelea kuwabatiza watu na kuhubiri. Manz alikuwa mwaminifu na mtiifu na hakuruhusu ukweli huo wa ubatizo kupotea hata ingawa alikumbana na pingamizi nyingi.

Hapo Disemba 3, 1526 Manz alikamatwa tena na kufungiwa huko korokoroni Wellenberg. Na hapo January 5, 1527 yeye alihukumiwa afe kwa kuzamishwa majini. Basi kifo cha kuzamishwa majini kikaja kujulikana kama "ubatizo wa tatu." Wakati Manz alikuwa akiongozwa kuelekea mto Limmat yeye alipaza sauti na kumsifu Mungu huku akiwashuhudia umati uliokusanyika. Mtumishi mmoja wa injili akaambatana naye huku akimhimiza kukana imani yake. Lakini kwa umbali mama yake na ndugu zake walimhimiza kusimama wima na kuteseka kwa ajili ya Bwana Yesu. Basi mikono ya Manz ikafungwa na kuvutwa hadi hapo katikati mwa magoti yake na kijiti kikawekwa kati ya magoti hayo ili asiwe na uwezo wa kufanya lolote. Ndipo akainamishwa na kutupwa majini na kuzama majini kama Anabaptisti wa kwanza kabisa kuifia dini yake. Inasemekana kwamba maneno yafuatayo ndio yalikuwa ya mwisho ya Manz: "Mikononi mwako E Mungu naiweka roho yangu."

Basi ukweli kuhusiana na ubatizo wa muumini haukutufikia kwa bei rahisi. Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya kururudishia ukweli huo mkuu kwa njia ya wale ambaao walikuwa tayari kutoa uhai wao kwa ajili ya kudumisha ukweli huo. Tunaomba kwamba kanuni hii ya ubatizo itazidi kudumishwa na kuheshimiwa katikati mwa watu wa Mungu.

—mws

UKWELI WA INJILI

Gazeti la "Ukweli wa Injili" huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambaao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaoletha na utakaso wa Yesu Kristo; ambaao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayewmongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamiletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinafsi na wa upendo ambaao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

UAGIZAJI

Ukweli wa Injili ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anavyotuongozoa. Tudembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili uagize jalida hili kuititia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambaao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

WASILIANA NASI

Gazeti a Ukweli wa injili linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kuititia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

Ukweli wa Injili, 605 Bishops Ct., Nixa, MO 65714 USA

editor@thegospeltruth.org

Tahariri



Nikintumikia Bwana kwa unyenyekevu wote . . . —Matendo 20:19a.

Miaka mingi iliyopita ililikuwa jambo la ajabu mtu kushuhudia watu elfu tatu wakibatizwa kama katika Siku ya Pentekoste. Tazama kulivyokuwa na msururu mrefu wa waumini wapya, wote wakingojea kwa hamu ili nafasi yao ya kuingia majini ifike. Tazama jinsi watu hao walivyojaa tabasamu na jinsi furaha iliviyowajaa huku miyo yao ikibubunjika kwa nyimbo. Na tazama jinsi sifa zaokwa Mungu ziliviyotoka kinywani mwao, na jinsi walivyoinua mikono yao juu kuelekea mbinguni huku wakimwabudu Bwana Yesu. Ni dhahiri kwamba wote ambao walikuwa wamemkataa Yesu na kushuhudia tukio hilo waliadhiriwa sana na tukio hilo.

Mimi ninamshukuru Mungu kwa sababu maisha yangu yalibadilika sana kutokana na wokovu ambao nilipokea huku nikiwa ningali mtoto mdogo, na hapo baadaye nikazikwa majini pamoja na Kristo kwenye ubatizo. Zaidi ya hayo, mimi nimekuwa na mweke mkuu maishani mwangu wa kubatiza watu wengi: nilishawahi kubatiza watu katika mto wa Kiafrika ambamo mamba waliishi, kubatiza watu katika maji yaliyojaa minyoo, kubatiza watu katika maji ambayo yalisimama mahali moja na kujaa matope, kubatiza watu katika mito safi iliyojaa maji yanayoteremka kuelekea ziwani, kubatiza watu kwenye mfereji wa maji huko Pakistani, na katika ziwa baridi sana huko Kanada, na hata kwenye sehemu za ubatizo ndani mwa makanisa mengi madogo. Hata ingawa ubatizo haufanywi kuwa wa kiroho zaidi kutokana na mahali ambapo ubatizo huo unafanyiwa, mimi huwa na furaha kubwa wakati ambapo ubatizo unafanyiwa mahali pa kawaida huko nje kwenye mto ambako kila mtu anaweza shuhudia tukio hilo.

Katika robo hii ya mwaka nimekuwa na mzigo mkubwa moyoni mwangu wa kushiriki kweli kadhaa kuhusiana na swala la ubatizo. Moyo wangu umejaa shukrani kutoka na kweli na mwangaza ambao tungali tuko nao hata katika siku hizi zetu. Ubatizo ni jambo muhimu lakini mimi nimeona kwamba katii ya watu wa Mungu kumeanza kuingia upungufu wa ari na shauku ya kufanya ubatizo. Lakini ubatizo haustahili kuwa jambo la baadaye au jambo la kushtukia baada ya mtu kuokoka. Ubatizo unastahili kuwa katii ya mambo ya kwanza kabisa ya kutii baada ya mtu kuokoka. Ni ombi letu kwamba Roho wa Mungu ataleta mwamsho mpya katikati mwa watu wa Mungu ili umuhimu na urembo wa fundisho hili kuhusiana na ubatizo na mazoea yake ung'are kanisani.

Ndugu Ulysses Phillips ambaye alikuwa mwandishi wa nyimbo aliandika na kusema: "Natangaza ufulufuo, ufulufuo moyoni mwako; nimefufuka toka kwa wafu, na badala yake sasa naishi na Yesu . . . Twamshukuru Mungu kwa ushindi, Yeye alinitoa mautini akaniinua nikapata uhai; kwa upendo na nguvu zake za kiungu, uhai wa milele sasa ni wangu." Wimbo huo unaeleza waziwazi kuhusu ushuhuda na maaana ya ubatizo.

Ni ombi letu kwamba kila msomaji atapata faraja na uamsho mpya akitafakari kuhusu urembo na ukweli ambao unaashiriwa na ubatizo.

Michael W. Smith

Oktoba 2014



**"Ubatizo wangu katika mto wa Santiam,
huko Oregon Marekani."**

mengi kwa
MTANDAO

Tutembelee kwa
www.thegospeltruth.org

ili uagize na kusoma
jarida letu.



Mahali pa Ukumbusho

Wakati mwingu katika nyakati za Agano la Kale watu walitengeneza madhabahu kwa Mungu baada ya wao kupata ushindi wa aina fulani, au baada ya Bwana kuwatembalea. Madhabahu hayo yalikuwa mahali pa ukumbusho kuhusu mambo yale ambayo Mungu alikuwa amewafanya.

Ubatizo unastahili kuwa mahali maalum pa ukumbusho kwa kila mtoto wa Mungu. Wakati Shetani amekuletea majaribu na kufanya vita na maisha yako ya kiroho linakuwa jambo la baraka kubwa mtu kukumbuka tendo la kumtii Mungu ambalo ye ye alifanya wakati alishiriki kwa njia ya uwazi kabisa katika tendo la kuzikwa majini na kufufuka tena katika ubatizo na kujitambulisha na Bwana Yesu. Mahali hapo pa ukumbusho panakuwa chanzo cha nguvu na ushindi dhidi ya adui Shetani.

MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

SOMO: UBATIZO WA MAJI

Somo la Biblia: Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu —(Mathayo 28:19).

Muhstasari: Waumini wa Yesu Kristo wameamuriwa kubatizwa kwa maji. Tendo hili la kumtii Yesu kwa kuingizwa ndani ya maji linaashiria kifo, kufufuka, na maisha ya kiroho ambayo yamebadilika kutokana na utakaso wa damu ya Yesu.

Maana ya Ubatizo: Neno ubatizo linatokana na neno la Kiyunani baptizo ambalo maanak yake ni kuingiza ndani ya maji, kutumbukiza, kuingiza mwili wote, maanake maji kujaa hadi kumzidi mtu.

I. Amri ya Kiungu

- A. Marko 16:15-16 Wabatizeni waumini wote.
- B. Matendo 2:38 Petro aagiza watu wabatizwe.

II. Yohana Alifunza kuhusu Ubatizo / Yesu Alitoa Mfano Mzuri wa Ubatizo

- A. Marko 1:4-5 Yohana anahubiri ubatizo wa toba.
- B. Mathayo 3:16-17 Yesu anabatizwa na Yohana Mbatizaji.

III. Kanisa la Kwanza Lilikuwa na Mazoea ya Kubatiza Waumini

- A. Matendo 2:41 Siku ya Pentekoste.
- B. Matendo 8:12 Waumini wa Samaria.
- C. Matendo 8:35-39 Mtu wa Kushi.
- D. Matendo 9:17-18 Mtume Paulo.
- E. Matendo 10:44-48 Nyumba ya Kornelio.
- F. Matendo 16:14-15 Lidia wa Thiatira.
- G. Matendo 16:30-33 Mlinzi wa gereza.
- H. Matendo 18:8 Wakorintho.
- I. Matndo 19:1-7 Wanafunzi wa Efeso.

IV. Ubatizo ufanywe “Kwa Jina La”

- A. Mathayo 28:19 Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.
- B. Matendo 2:38 Kwa jina la Yesu Kristo.
- C. Matendo 10:48 Kwa jina la Bwana.

V. Matakwa ya Ubatizo

- A. Matendo 2:38 Toba.
- B. Matendo 2:41 Pokea Neno.
- C. Matendo 8:37 Kuamini.
(tazama pia Marko 16:16; Matendo 8:12; 18:8)

VI. Ubatizo Unaashiria Nini?

- A. Warumi 6:3-4 Kifo, kuzikwa, na kufufuka.
- B. Wakolosai 2:12 Kuzikwa na kufufuka pamoja na Kristo.

VII. Kuingizwa Kabisa Majini

- A. Maana ya baptizo.
- B. Marko 1:5 Kubatizwa mtoni.
- C. Yohana 3:22-23 Yohana alibatiza mahali ambapo kulikuwa na maji mengi.
- D. Matendo 8:38 Filipo na Towashi wakaingia majini.

VIII. Kusudi la Ubatizo

- A. 1 Petro 3:21 Ushuhuda wa dhamiri safi.
- B. Matendo 2:41-42 Kujitambulisha na kanisa.

Tamati:

Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza. Kisha, walipopanda kuto-ka majini...yule towashi...alikwenda zake akifurahi.

—Matendo 8:38-39

UBATIZO WA MAJI

Nakala ya kuandamana na mafunzo ya Biblia

YESU ALITOA MFANO BORA

Yohana Mbatizaji alimtumbukiza Yesu majini wakati alipombatiza. Yesu alipozinduka kutoka majini mbingu zilifunguka na Roho Mtakatifu akamshukia kama njiwa. Nayo sauti ikanena toka Mbinguni: "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye" (Mathayo 3:15-17). Kati ya maneno ya mwisho ambayo Yesu aliwambia wanafunzi wake yalikuwa maagizo kwamba waenende na kufundisha mataifa yote na kuwabatiza (Mathayo 28:19-20).

UBATIZO NI KANUNI YA KANISA

Kuna tamaduni chache sana za kutoa ushuhuda ambazo zinapatikana katika Agano Jipy. Ubatizo ni ishara ambayo ilitokana na amri ya Kristo, ambaye pia alitoa mfano bora wa jambo hilo. Basi ubatizo ni moja ya kanuni tatu ambazo Wakristo wameamuriwa kufuata katika kipindi hiki cha Agano Jipy.

Ubatizo ni jambo ambalo limekaribiana sana na kazi ya wokovu, kazi ambayo ni ya kiungu: "Aaminiye na kubatizwa ataokoka" (Marko 16:16). Shauku la Mungu ni kwamba kila anayetubu apate kubatizwa. Katika siku ya Pentekoste watu walio-okoka walimuuliza Petro kile ambacho walistahili kufanya baada ya wao kushawishika kwamba walikuwa wenye dhambi: "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu..." (Matendo 2:37-38). Ubatizo silo jambo la kuchukuliwa hivi hivi, mbali ni jambo ambalo linastahili heshima kwa kuwa ni kanuni ya kiungu kutoka kwa Bwana.

MIFANO YA UBATIZO KATIKA BIBLIA

Kanisa la kwanza lilitundisha na kufanya ubatizo. Katika siku ya Pentekoste karibu watu elfu tatu waliokoka na kubatizwa (Matendo 2:41). Naye Filipo aliwhabiria watu wa Samaria na wake kwa waume wakaokoka na kubatizwa (Matendo 8:12). Naye mtume Paulo alibatizwa muda mfupi tu baada ya yeze kuokoka katika barabara hiyo ya kuelekea Dameski (Matendo 9:17-18). Nao watu wa Nyumba ya Korinelio, ambao walikuwa ni watu wa mataifa, walifuata mfano wa Bwana Yesu kuhusiana na swala la ubatizo (Matendo 10:44-48). Zaidi ya

hayo, watu wa Korintho ambao waliweza kutubu walibatizwa. Hata nao wanafunzi wa huko Efeso wakabatizwa. Naye askari wa gereza ambaye alikuwa amesimamia Paulo na Sila, baada ya yeze kutoa maisha yake kwa Yesu, aliokoka na kubatizwa usiku huo huo (Matendo 16:30-33). Na kwa kweli hata baada ya miaka elfu mbili ubatizo wa aina hio ungali unafanywa na wafuasi wa kweli wa Bwana Yesu Kristo.

KUMTUMBUKIZA MTU MAJINI

Yesu aliwaagiza wanafunzi wake wabatize watu "kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu" (Mathayo 28:19). Kumtumbukiza mtu majini kwa jina moja la Utatu wa Mungu ni jambo ambalo linakubaliana na maagizo ya Kristo kuhusiana na kitendo hicho cha kuwabatiza waumini.

UBATIZO NI WA WAUMINI PEKE YAO

Lakini ubatizo haustahili kufanya kwa watoto na pia haustahili kufanya kwa wale ambao hawajaokoka, wale ambao wanajaribu kuwa washirika wa kanisa bila kuokoka. Maandiko yamefundisha "ubatizo wa waumini." Mtu anahitaji



*"Aaminiye
na kubatizwa
ataokoka."
Marko 16:16*

kutubu dhambi zake na kuokoka kabla ya kubatizwa. Wale ambao walibatizwa katika Siku ya Pentekoste walikuwa wale ambao walikuwa wamepokea Neno la Bwana. Basi ubatizo umeshikanishwa sana na mtu kumwamini Yesu. Wakati Filipo alishiriki Injili na mtu yule wa Kushi, mtu huyo aauliza: "ni nini kinachoniuza nisibatizwe?" Naye Filipo akamjibu, "Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana" (Matendo 8:36-37). Kutubu na mtu kuamini nguvu za Bwana Yesu, ambazo zina uwezo wa kuokoa, ni mambo ambayo mtu anastahili kuwa nayo ili aweze kubatizwa. Kama mtu haamini na kutubu kwanza, basi ubatizo wake hautakuwa na maana yoyote. Basi ni jambo la kupotosha ukweli na hata kupoteza kusudi la

(Inaendelea kutoka ukurasa 6)

(Endelea kutoka ukurasa 5)

ubatizo wakati ambapo sisi tunawabatiza watoto wachanga na pia kuwabatiza wale ambao hawajaamini. Kwa kufanya hivyo tunawapatia tumaini kwamba wanaweza kupata wokovu kwa njia ya ubatizo.

UBATIZO HAUMWOKOI MWENYE DHAMBI

Ubatizo wa maji hauondoi dhambi maishani mwa mtu. Hakuna utakaso wa kiroho unaopatikana kutoptana na ubatizo. Ni “damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote” (1 Yohana 1:7). Mtu ambaye hajaokoka kama atabatizwa atatoka majini akiwa mwenye dhambi kama alivyokuwa akiingia majini.

Wokovu na utakaso wa moyo unatokana tu na neema ya wokovu wa kiungu kupitia kwa damu yake Kristo. Hata mtu anaweza kubatizwa mara ishirini lakini awe mwenye dhambi kama alivyokuwa hapo mbeleni ikiwa hatakuwa na ujuzi wa kuzaliwa kwa njia ya kiroho. Kama mtu hatakuwa kwa ajili ya dhambi ubatizo wake unakuwa sherehe ya bure ambayo haina maana yoyote.

ISHARA YA KIFO NA KUFUFUKA

Ubatizo ni ishara ya kifo, kuzikwa, na pia kufufuka kwa Bwana Yesu. Ni sherehe ambayo inawakilisha mabadiliko yanayofanyika maishani mwa mtu ambaye amezaliwa tena: “Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima” (Warumi 6:3-4). Wakati mtu anatumbukizwa majini, jambo hili linawakilisha kuzikwa kwake kwa njia ya kiroho. Maisha yake ya kale, yaani maisha ya dhambi, yanazikwa. Lakini anapotoka majini jambo hili linawakilisha maisha yake yaliyofufuka, maisha ya uhuru kutoptana na dhambi ndani yake Yesu Kristo. Walakini, hakuna utakaso ambao unafanyika hapo majini. Hii ni ishara na ushuhuda wa utakaso ambao umefanyika hapo mbeleni kupitia kwa damu ya Yesu. Mtu anawekwa muhuri wa Mungu kutoptana na yeze kutii Neno la Mungu.

UBATIZO NI KUTUMBUKIZA MTU MAJINI

Neno la kibiblia “ubatizo” linatokana na neno la Kiyunani baptizo. Maana yake ni kuingiza ndani ya maji, kutumbukiza, kuingiza mwili wote majini. Maana hiyo ni ushahidi kwamba ubatizo unaofundishwa kwenye Bibia ni wa kumwingiza mtu majini kabisa kabisa. Makundi mengi ya kidini hunyonyizia mtu maji au kumwangia mtu maji katika ubatizo. Lakini hili ni jambo lililo kinyume na Maandiko na mpango wa Yesu. Kumwagia mtu maji ama kunyonyizia ni jambo lisilofikia kiwango cha ishara ya urembo wa ubatizo. Kumwingiza mtu majini mwili wote ndilo jambo linalowakilisha mabadiliko yote ya maisha ambayo mtu hupata kupitia kuzikwa kwake na kufufuliwa pamoja na Kristo.

Katika nyakati za Biblia Wakristo walifundishwa kwamba walihitaji kutumbukizwa majini kabisa kabisa. Yohana Mbatizaji alibatiza watu katika mto wa Yordani (Marko 1:5). Andiko la Yohana 3:22-23 linasema kwamba Yohana alibatiza watu mahali ambapo palikuwa na maji mengi. Lakini maji mengi

hayahitajiki wakati ambapo watu wananyonyiziwa au kumwagiwa maji kidogo. Filipo na towashi nao “wakatelemka wote wawili majini” (Matendo 8:38). Lakini mfano mkubwa kabisa wa jambo hili ulikuwa ni Kristo, ambaye alitumbukizwa majini mzima mzima (Mathayo 3:16-17).

USHUHUDA WA NJE WA KAZI INAYOFANYIKA NDANI YA MTU

Ubatizo ni ushuhuda wa nje wa kazi ya Mungu inayofanyika ndani ya mtu. Ubatizo ni “jibu la dhamiri safi mbele za Mungu” (1 Petro 3:21). Ubatizo haumpatii mtu dhamira safi, bali ni tendo la kutii na ni tamshi la mtu la kuwa wazi mbele zake Mungu. Watu ambao wanamfuata Bwana katika ubatizo wanatangaza mbele ya watu wote kwamba wao ni viumbe mpya ndani yake Kristo na kwamba sasa wao ni sehemu ya jamaa ya Mungu. Ubatizo ni njia ya mtu kukiri hadharani kwamba yeze sasa ni muumini wa Kristo, na ni jambo la ajabu linaloonekana na wanadamu, ambalo linadhihirisha kwamba mtu huyo ni mpya ndani ya Kristo—kwamba yeze sio tena mtumishi wa dunia bali ni mwana wa Mungu.

—mws



Nikiwabatiza waumini katika mfereji wa maji huko Pakistani

MASWALI na MAJIBU

1. Je, watu wanaweza kufika Mbinguni kama hawajabatizwa?

"Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezি
kuona ufalme wa Mungu" (Yohana
3:3). Watu ambao wataingia Mbinguni
ni wale ambao wamezaliwa mara ya pili
na kuokoka kwa neema ya Mungu. Sisi
hatuokolewi kutokana na matendo yetu
au kwa kufuata mambo ya sherehe
(Waefeso 2:8-9). Kwa hivyo, lile tendo la
kubatizwa kwa mwili halituokoi. Kwa
kweli kutakuweko na watu Mbinguni
ambao hawakubatizwa kwa maji, lakini
wao watakuwa wamesamehewa
dhambi zao kuititia kwa damu ya Yesu.

Mfano bora wa jambo hilo ni yule mwizi
ambaye alikuwa pale msalabani: "Kisha
akasema, Ee Yesu, nikumbuke
utakapoingia katika ufalme wako. Yesu
akamwambia, Amin, nakuambia, leo hivi
utakuwa pamoja nami peponi" (Luka
23:42-43). Mwizi huyou aliokolewa
msalabani na hakuwa na nafasi ya
kupata ubatizo. Yesu alimkubali na
kusema kuwa atakuwa naye peponi
(paradiso). Kuna watu ambao huwa na
wakati wa kuomba ili wapate wokovu,
lakini pengine hawana mweke katika
maisha haya, au hawako katika hali ya
kimwili ya kuweza kubatizwa. Wao
hawatazuiwa kuingia mbinguni.

Lakini mtu kuchagua kwamba
hatabatizwa ni tendo la kukosa utiifu
ikiwa yeye ana nafasi ya kupata ubatizo.
Hii atakuwa ni dhambi ambayo
itamfanya mtu kupoteza wokovu wake.

2. Je, mtu anastahili kubatizwa tena ikiwa atatoka kanisa la uwongo na kuingia katika ushirika wa kweli wa watu wa Mungu?

Katika Mathayo 28:19 ni wazi kwamba
Yesu aliwafunza wafuasi wake kubatiza
"kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho
Mtakatifu." Petro akawaambia watu
hao katika Siku ya Pentekoste
"mkabatizwe . . . kwa jina lake Yesu
Kristo" (Matendo 2:38). Lakini Petro
akizungumza katika nyumba ya
Kornelio alisema "abatizwe kwa Jina
lake Yesu Kristo" (Matendo 10:48).
Yeye hakuwa akisema kinyume na
mafundisho ya Yesu, bali alikuwa
akitenganisha ubatizo wa Wakristo
kutokana na ubatizo wa aina nyingine
ambao ulikuwa ukifanyika nyakati
hizo. Zaidi ya hayo, na pengine jambo
ambalo ni muhimu zaidi, ni kwamba
wengi wa watu wa wakati huo



Malawi, Afrika

walimwamini Mungu lakini
wakamkataa mwana wake Yesu;
ndiposa Petro alikazia swala la mtu
kubatizwa kwa jina la Yesu ambaye
ndiye utimilifu wote wa Mungu kwa
njia ya kimwili (Wakolosai 2:9). Wale
ambao mwanzoni walimkataa Yesu
waliamuriwa kutangaza imani yao
hadharani, kwamba Yesu ni Mwokozi
na kwamba wao sasa ni wafuasi wa
Kristo.

Basi mafundisho ya Petro hayakuwa
kinyume na mafundisho ya mtu
kubatizwa kwa majina ya Utatu wa
Mungu, lakini mafundisho yake yalitilia
mkazo jambo lile ambalo mbeleni
halikutiliwa maanani. Basi ni jambo

linalofaa na la kimaandiko mtu
kubatizwa kwa jina la Baba, la Mwana
na la Roho Mtakatifu.

3. Je, mtu anastahili kubatizwa tena ikiwa atatoka kanisa la uwongo na kuingia katika ushirika wa kweli wa watu wa Mungu?

Kama ubatizo haulingani na "ubatizo wa
waumini" basi ubatizo kama huo
haukuliani na maandiko. Kubatiza
watoto au mtu kubatizwa huku akiwa
na dhambi maishani mwake ni jambo
ambalo ni kinyume na kusudi kamili na
ushuhuda unaokusudiwa na ubatizo.
Basi mtu anastahili kubatizwa tena
ikiwa itafika wakati ambapo ataokoka
vizuri kutokana na dhambi zake na awe
amepata ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili.

Wokovu ndio kitu ambacho humleta
mtu kwa Kanisa la Mungu na kwenye
ushirika na watu wa Mungu. Hata
ingawa ubatizo wa muumini
umefanyika wakati ambapo muumini
huyo ni mshirika wa dhehebu la
uwongo Mungu huheshimu kitendo
hicho cha kutii wakati ambapo Yeye
anafanya kazi yake ya wokovu. Wakati
watu wameondoka kutoka dhehebu la
uongo ili wawe na ushirika na watu wa
kweli wa Mungu, mara nyingi wao huwa
na shauku la kuukana mpango wa dini
ambayo wao walikuwa washirika.

Sehemu moja ya ushuhuda huo wa
kukataa dini hiyo ya uwongo inaweza
kuwa kwa njia ya wao kubatizwa tena.
Hata ingawa Biblia haijatoa maagizo ya
aina hiyo, ni jambo linaloleweka ni
kwa nini mtu angetaka kutangaza uhuru
wake hadharani kwamba yeye ameacha
dhehebu la uongo. Swala la mtu
kubatizwa tena baada ya yeye kuacha
dhehebu la uongo ni uamuzi ambao kila
mtu anastahili kuachwa afanye
kulingana na jinsi anavyoongozwa na
Roho Mtakatifu.

—mws



JE, WAJUA?

Ubatizo wa maji halikuwa jambo mpya kwa Wayahudi wakati Yohana Mbatizaji alianza kuhubiri ubatizo wa toba. Katika wakati wa Agano la Kale ubatizo ulikuwa ni jambo la kisherehe la kuonyesha kwamba mtu ameongoka na kuingia dini ya Uyahudi. Makafiri wangefanyika kuwa washirika wa dini ya Kiyahudi kwa ubaizo ili wawe sehemu ya watu wa Israeli na kutambulika pamoja nao.



Wape Maonyo

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA
Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

Mwanadamu, nimekuweka kuwa mlinzi wa nyumba ya Israeli; basi, sikia neno hili litokalo katika kinywa changu, ukawape maonyo haya yatokayo kwangu. –Ezekieli 3:17

Kama wewe ni mhudumu wa kweli wa injili Mungu amekuweka kama mlinzi wa watu wake. Wewe ni askari mlinzi wa kuisimamia na kulinda huduma ambayo Bwana amekuweka ili kuitunza. Huduma yako sio kazi ya kawaida bali ni mwito kutoka kwa Mungu na inahitaji kujitolea kwako kwa watu ambao Mungu amekupatia. Hebu msikilize Roho wa Mungu na uruhusu Neno la Mungu kuwa nambari moja kwa yote ambayo unafundisha na kuhubiri.

Wakati adui yumo kazini mwake na watu wako wawe kwenye hatari kazi yako ni kuwaonya katika Bwana. Wewe usiogope kutahadharisha watu na pia usiogope kumdhihirisha adui. Lakini watu hupenda kusikia maneno yale yanayofawarizji na kuwajenga. Mambo hayo pia ni muhimu, lakini wewe pia usipuuze maonyo ya kiungu. Familia nyingi na hata makusanyiko mengi ya Wakristo wameingiza uwongo kwenye ukweli kwa sababu wahudumu wa Injili wamepuuza jukumu lao la kutoa onyo.



Wewe ni balozi wa Kristo, mwakilishi wa Mungu. Kazi yako ni kulisha, kufunza, kutahadharisha, na hata kuwaonya kusanyiko la Mungu. Wapende watu wa Mungu na ujitlee mhanga kuwatuumikia. Kuwa mfano bora kwao wa utakatifu na usafi. Wakati majaribu yanakuwa moto sana na mambo ni magumu kumbuka kwamba wewe ni mhudumu wa Bwana. Yeye atasimama na wale walio wake na atakusaidia na kukupa nguvu wakati ukiendelea kuwa mwaminifu.

—mws